

**HOTUBA YA BALOZI DR. SALIM AHMED SALIM
WAKATI WA SHEREHE ZA UZINDUZI WA MAJENGO
YA MAPYA YA SHULE YA MWALIMU
JULIUS KAMBARAGE NYERERE
TAREHE 5 JANUARI 2002**

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Habari Corporation,
Mwenyekiti wa Kamati ya shule,
Waheshimiwa Mabalozzi,
Wageni Waalikwa,
Wazazi,
Waalimu,
Wanafunzi,
Mabibi na Mabwana,

1. Shukrani kwa Mwaliko:

- 1.1. Kwanza naomba nianze kwa kuwashukuru Viongozi wa shule - Kamati ya Shule, Walimu na Wanafunzi kwa kunipatia fursa hii ya kukutana na kushiriki pamoja nanyi katika uzinduzi wa majengo mapya ya shule hii.

2. Historia ya Shule, Mafanikio na Pongezi:

- 2.1. Nimejulishwa kwamba shule hii haina muda mrefu tangu ilipoanzishwa katika mtaa wa Malongwe, Mwananyamala takriban miaka saba hivi iliyopita. Katika kipindi hicho shule imeweza kuongeza idadi ya wanafunzi kutoka wanafunzi 32 hadi kufikia wanafunzi 420 ongezeko la zaidi ya mara 10. Idadi ya walimu nayo imeongezeka kwa karibu kiwango hicho hicho kutoka walimu 6 mwaka 1997 hadi 27 waliopo hivi sasa.
- 2.2. Napenda niwapongeze Bodi ya Habari Corporation na Kamati ya shule kwa kufanikiwa kuandaa mazingira ya shule ambayo yameiwezsha kuwa kivutio kwa walimu wazuri na wenye sifa kukubali kufanyakazi katika shule hii licha ya uchanga wake

na sina shaka ni kutokana na ubora wa kazi za walimu hawa shule imeweza kujijengea sifa na umaarufu hatakuwa kivutio kwa wazazi. Ninawapongeza wote kwa mafanikio mliyoyapata na ninawataka msilegeze kamba ili mpate mafanikio makubwa zaidi.

3. Elimu ni Ufunguo wa Maisha Lengo liwe Elimu Bora:

- 3.1. Sina haja ya kusisitiza kwenu nyie wazazi wa wanafunzi hawa wa shule ya Mwalimu Julius K. Nyerere umuhimu wa elimu. Uamuzi wenu wa kujinyima kile kidogo mlichu nacho ili watoto wenu wapate elimu iliyobora ni thibati tosha kuwa mnatambua hilo. Labda tunaweza tukatofautiana tu kuhusu tafsiri ya nini hasa maana ya elimu bora. Si nia yangu kuingia katika undani wa mjadala huo. Kwetu sisi inatosha kukubaliana kwamba elimu bora ni ile inayomwezesha mtu kuyaelewa na kuyamudu mazingira yanayomzunguka. Katika kila ngazi elimu haina budi kulenga kumuongezea yule anayeipata uhuru kwa kumkomboa kutoka hali ya kuwa mtumwa wa mazingira na badala yake kumuongezea uwezo wa kuyatawala katika jitihada za kujiletea maendeleo. Kwa tafsiri hii kigezo cha jumla cha ubora wa elimu ni kiwango ambacho elimu hiyo inatuongezea uwezo wa kujitegemea.
- 3.2. Suala la elimu ya kujitegemea lina umuhimu wa pekee katika dunia ya leo. Lina maana ya kutilia mkazo elimu ya jumla yenye lengo la kupanua upeo wa kuelewa dunia kupitia maarifa tunayopata katika fani mbalimbali. Lakini vilevile elimu inayotilia mkazo sayansi na teknolojia katika kuumba vitu na zana mbalimbali. Elimu ya kujitegemea kwa maana hiyo ni elimu inayotoa fursa ya mwingiliano wa nadharia na vitendo.
- 3.3. Ninafurahi kuwa hili ni lengo lenu kubwa la kutoa elimu bora kwa vitendo vinavyoongozwa na nadharia sahihi na vitendo vyenyewe kusaidia

kurutubisha na kuboresha nadharia. Ninawatakia kheri na mafanikio katika azma hiyo.

4. Tulienzi Jina la Mwalimu kwa Kusisitiza Elimu na Kupiga Vita Maovu:

- 4.1. Jina la shule hii ni Mwalimu Julius K. Nyerere. Ni jina zito na lenye nafasi ya pekee katika historia ya ukombozi wa nchi yetu na wa Bara la Afrika. Mchango wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere katika kuikuza falsafa na nadharia ya elimu kwa jumla na dhana ya elimu ya kujitegemea unatambulika duniani kote. Aidha nimeambiwa kuwa jiwe la msingi la majengo haya tunayoyazindua leo liliwekwa na Mama Maria Nyerere. Yote mawili yana umuhimu wa kipekee kwa watanzania. Ni majina ambayo ni kielelezo cha yale yaliyomema kwa taifa letu. Kwa kuhusishwa nayo shule imebeba dhamana kubwa kuwa itadumu kuwa kielelezo cha maana halisi ya elimu ya kujitegemea kifikra na kwa matendo ya wahitimu wake.
- 4.2. Hii ni changamoto si tu kwa wanafunzi wa shule ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere bali ni changamoto kwetu sote; wazazi, walimu, wajumbe wa kamati ya shule na wajumbe wa Bodi ya Habari Corporation.
- 4.3. Naomba nimalizie nasaha zangu kwa kuwapongeza viongozi wa Kampuni ya Ujenzi ya Masasi (Masasi Construction Company Ltd) kwa kazi nzuri waliyoifanya katika muda huo wa miezi sita. Mmedhihirishia jamii kuwa tunao uwezo wa kufanya mazuri tukidhamiria. Nanyi nawatakia mafaniko zaidi.

AHSANTENI KWA KUNISIKILIZA.